



NI FAHARI KUTAFSIRI

Je unamfahamu mtu mwenye matatizo ya kuzungumza Kiingereza? Hali hiyo inawazuia wasiweze kupata taarifa au huduma wanazohitaji? Labda hawajisikii vizuri kutegemea familia au marafiki kuwasaidia katika kuzungumza? **Kama ni hivyo, mkakati wa nembo ya “Happy to Translate” (Ni Fahari Kutafsiri) unalenga kusaidia!**

NEMBO YA “HAPPY TO TRANSLATE” NI NINI?

Nembo ya “Happy to Translate ” inaonyesha mafanikio ya mawasiliano baina ya watu wawili ambao hawazungumzi kwa lugha moja. Mchoro ulichaguliwa na jamii mbalimbali za Scotland kwa kura ya maoni ya walio wengi. Mkakati huu unafanywa ili kusaidia kuboresha ubora wa maisha ya watu Scotland ambao huongea au kuandika Kiingereza kidogo au hawajui Kiingereza kabisa au wanaotumia lugha isiyokuwa ya matamshi. Mashirika yanayoonyesha nembo hii yatatoa msaada wa lugha kwa njia ya huduma ya siri ya kutafsiri na kukalimani.

KUTAFSIRI NA KUKALIMANI NI NINI?

Kutafsiri - maneno yaliyoandikwa yanabadilishwa kutoka lugha moja kuwa nyingine.

Kukalimani - watu wawili au zaidi ambao hawatumii lugha moja wanaongea kwa msaada wa mtu wa tatu mwenye ujuzi fasaha wa lugha zote mbili. Wataalamu wa kutafsiri maandishi na wakalimani ni mabingwa wa lugha waliopatiwa mafunzo maalum. Wanafungwa na kanuni za maadili na viwango vya ubora ambavyo huhakikisha kuwa kazi zao ni sahihi, hazina upendeleo, za kuwajibika na siri. Wengine pia hubobea kwenye lugha stadi zinazotumika kwenye maeneo kama ya sheria na utabibu.

JE NEMBO YA “HAPPY TO TRANSLATE” ITASAIIDIA VIPI?

Wakati mteja ambaye anazungumza au kuandika Kiingereza kidogo au hajui Kiingereza kabisa anapotembelea shirika lenye nembo ya “Happy to Translate”,

SWAHILI

SWAHILI

mfanyakazi atafuata hatua chache rahisi kuamua ni lugha gani mteja anapendelea kutumia, na taarifa gani au huduma wanayohitaji. Hii ni pamoja na kumtaka mteja aonyeshe lugha yake kwenye orodha ya lugha au kutumia huduma ya lugha kwa simu. Mara lugha na mahitaji vikiisha julikana, miadi hufanywa kwa niaba ya mteja pamoja na mkalimani stadi, au nyaraka kutafsiriwa kwenye lugha inayostahili (ucheleweshaji utapunguzwa ikiwa msaada wa dharura utahitajika).

LINI & WAPI HUDUMA HIZI HUPATIKANA?

Mashirika kadhaa ya umma yanaongoza nembo ya “Happy to Translate ” katika kipindi cha 2005-07. Kundi la kwanza linajumuisha idara zilizochaguliwa ndani ya **Halmashauri ya Jiji la Edinburgh, Polisi wa Lothian na Borders, Halmashauri ya Moray , NHS ya Lothian, na Trust, Hanover (Scotland) & Bield Housing Associations** (mashirika ya nyongeza yatatangazwa). Mwishoni mwa awamu ya majaribio, mashirika mengine yatahamasishwa kuomba uanachama wa kutumia nembo ya “Happy to Translate” . Inatumainiwa kuwa baada ya muda, nembo itatumiwa kwa wingi na mashirika ya umma na binafsi ya Scotland ili kuboresha upatikanaji wa taarifa na huduma.

TAARIFA ZAIDI

Iwapo unamjua mtu yeyote anayeweza kufaidika kutokana na nembo ya “Ni Fahari Kutafsiri”, tafadhali mpe taarifa hii. Kwa tafsiri katika lugha za ziada au kwa miundo mingine (kama maandishi ya wasioona, kanda za kunasia sauti au maandishi makubwa) tafadhali piga simu 0131 444 4951 au andika kwa : “Happy to Translate” Logo Initiative, 12 New Mart Road, Edinburgh EH14 1RL. Kijitabu hiki pia kinaweza kupatikana kwenye tovuti ya www.happytotranslate.com.

**Kuimarisha nafasi sawa kwa kukabiliana
vyema na vizuizi vya lugha**